**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UZINDUZI WA MRADI WA KUIMARISHA UWEZO WA KUDHIBITI MAGONJWA YA MLIPUKO NA DHARURA ZA AFYA

**MWANZA: 13 Oktoba, 2025**

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatarajia kuzindua mradi mkubwa wa kitaifa wa kuimarisha uwezo wa Tanzania katika kuzuia, kujiandaa, kugundua, kukabiliana na kudhibiti magonjwa ya mlipuko na dharura nyingine za afya.

Mradi huu unaojulikana kama *"Pandemic Fund Project"* unatarajiwa kuzinduliwa tarehe 15 Oktoba, 2025 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko Jijini Mwanza, na utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wa maendeleo likiwemo Shirika la Afya Duniani (WHO), UNICEF, FAO na washirika wengine wa maendeleo.

Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya Dola za Kimarekani Milioni 25 ambazo ni sawa na Shilingi Bilioni 61.2 za kitanzania, aidha Kama ilivyo ainishwa mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano na Serikali ya Tanzania pamoja na wadau wa maendeleo ambapo nyongeza ya kiasi cha fedha za kitanzania bilioni 38.7 kutoka Serikalini na Wadau wa Maendeleo kitatumika pia kufanikisha malengo ya mradi huu.

Kupitia utekelezaji wa mradi huu, Serikali inalenga kuimarisha mifumo ya afya nchini kwa kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa na utambuzi wa mapema, kuimarisha maabara za uchunguzi wa vimelea vya magonjwa, kujenga uwezo wa wataalam na timu za dharura za afya, kuboresha uratibu wa dharura katika ngazi zote na kuimarisha mawasiliano ya hatari na ushirikishwaji wa jamii.

Utekelezaji wa mradi huu pia unaendana na juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha mfumo wa afya nchini na ni uthibitisho wa imani ya jumuiya ya kimataifa kwa uongozi wa Tanzania katika kuimarisha usalama wa afya na ustahimilivu wa mifumo ya afya.

Utekelezaji wa mradi huu utaimarisha ulinzi wa afya ya wananchi, kuongeza uthabiti wa jamii katika kukabiliana na dharura za afya na kuchangia moja kwa moja katika usalama wa afya wa kikanda na kimataifa.

Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatoa shukurani za dhati kwa wadau wote ambao tunashirikiana katika kuchangia na kutekeleza mradi huu ikiwa ni pamoja na wanajamii wote kwa ujumla.

Imetolewa na:

**Dkt. Grace Magembe**
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**